

THEODOROS WA PILI

**KWA NEEMA YA MUNGU, PAPA NA PATRIAKA WA ALEXANDRIA, MISRI YOTE
NA AFRIKA NZIMA, KWA WINGI WOTE WA KITI CHA KI-MITUME NA CHA
PATRIAKA, NEEMA NA REHEMA NA AMANI YA BWANA NA MUNGU NA
MWOKOZI YESU KRISTO, ALIYEFUFUKA TOKA WAFU.**

“Na tazama Mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.” (Mathayo 28:20)

Ndugu na dada zangu wapendwa,

Kwa maneno haya, na kwa ahadi hii yenye tumaini, Mwana wa Mungu alikamilisha kazi yake ya wokovu ulimwenguni. Yeye alitoka mbunguni akaja duniani ili kutupea wokovu. Yeye aliyekua maskini kwa ajili yetu. Yeye aliye kubali kutundikiwa msalabani na kuteswa mahala petu. Yeye aliye zikwa kwa ajili yetu. Yeye aliyefufuka kwa ajili yetu, na kifo kile alichovumilia kikawa mtangulinzi wa kutokufa.

Hata hivyo, timio hili halikuwa tu la maneno matupu, wala halikuwa tu la kihistoria. Ila, lilikuwa timio lenye upana na lisilo egemea wakati. Kanisa basi likafanyika mhusika mkuu wa ufufuo huu usioegemea wakati. Kanisa halikufanyika hivi kama tu dini iliyokita, bali kama Mwili wa Kristo, kama jamii ya watu wakosefu watafutao wokovu: watu wakubalio mwito wa Kristo: *“Njooi kwangu nyote msumbukao na mlio lemewa na mizigo nami nitawapumzisha” (Mat 11:28)*

Hatimaye Kanisa lilikuja kuwa ushahidi wa kweli jinsi Bwana aliye fufuka anatupenda. Kwa kuwa mtu aweza kuwa na tashwishi kwa jambo lolote, ila sio kuhusu upendo wa Mungu. Lakini ni jambo lipi litufanyalo kukaa mbali na Nyumba ya Baba? Ni kipi kitufanyacho kutorudi kwa Baba atupendaye na anaye tungojea? Yaweza kuwa ni kwa sababu tumeweka hakikisho letu kuu kwa nguvu zetu wenyewe? Ama ni kuona kana kwamba makosa yetu yamezidi kuliko upendo wa Mungu?

Chochote kiwezacho kuwa jibu kwa maswali haya, yafaa tuelewe kwamba umbali tulio nao baina yetu na upendo wa Mungu, unaashiria upungufu wa imani. Hii ni kwa ajili ya uhakika kwamba, tumaini na upendo hutuleta kwenye ushirika na Mungu, pindi tu inapoambatana na imani ya kweli. Tumaini na upendo huangazia njia ya kumrudia Mungu, ambapo tu tupo tayari kuungama, kama alivyofanya Petro: *“Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai” Mat 16:16.* Huu ni wakati tu imani inapokoma kuwa chemichemi ya kiburi, na kuwa chemichemi isiyopunguka ya matendo mema.

Ni huzuni kubwa kuwa siku hizi tumefikia kilele cha elimu, ila tumepungukiwa kwa elimu ya imani. Kiteknologia twaweza kuwa tumeelea ila kitheologia tumepungukiwa. Tumetenga

kando neno lililodhirishwa la Mungu, na kuamini injili jipya, kutoka kwa sayansi, filozofia na siasa. Tumemkana Mungu na kuamini kwamba hatumuhitaji ili kutambua kuwepo kwetu. Tumesahau imani ya kweli na kujipa kwa uwongo wa wakati wetu: ubinafsi, uwezo na utajiri.

Na sasa kwa majuto tunapogundua kuwa ulimwengu wetu umejawa na fikra potovu za walio na nguvu miongoni mwetu, sasa twaanza kutafuta njia ya wokovu. Na sasa kwa kuwa tumekuwa wapungufu kwa ujuzi wa upendo wa Mungu, tunajikaza kupata nguvu za kusema kuwa: *“Nitainuka niende nyumbani mwa Baba” Luka 15:18*. Hata hivyo, ufufuo wetu hauwezekani pasipo imani yetu kufanywa jipya. Kutojua kwetu kuhusu evangelia kutapona punde tu tutakapo lijua neno la Mungu.

Ndugu na dada zangu,

Karne ishirini na moja baada ya Mungu-Mtu kufufuka, na injili yake kuenea kwa mataifa yote, mwanadamu mara tena amejipata mbali sana na mapenzi ya Mungu. Njia ya pekee iliyo hakika ya kurudi nyumbani mwa Baba yetu ni kuhubiriwa upya imani. Na hii imani isiwe tu jambo la fikra tu, ila jambo lifanyikalo moyoni. Na iwe pia ukiri wa Kristo Yesu, aliye Njia, kweli na uhai. Imani hii iwe kama kazi ya kupeleka injili hadi mwisho wa dunia.

Hivi ndivyo tufanyavyo hapa Afrika, kwa sababu, kama alivyosema Yohana Kristostomu “.. hakuna mtu mwenye roho mbaya kuzidi mkristo asiye jali wokovu wa wengine” (P.G 60,162). Kazi hii yaweza kuwa kubwa na wafanya kazi wachache, ila roho zetu zapata joto kwa ahadi la tumaini la Bwana wetu kuwa *“milango ya jehanamu haitalishinda”* Kanisa (Mathayo 16:18). Ahadi hii ya tumaini ya Bwana ndiyo igeuzayo kazi hii iwe kazi ya upendo ushindao kifo. Kama vile tu Bwana wetu alivyo shinda Kifo kwa Ufufuko wake.

Kristo Amefufuka!

†THEODOROS WA PILI

Papa na Patriaka wa Alexandria na Africa Yote

Katika Mji Mkuu wa Alexandria

Pasaka Takatifu 2017